

Ujumbe wa Krismasi 2009

Kutoka kwa Katibu Mkuu wa Baraza la Mekanisa Ulimwenguni

Naye ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote. Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana; ikiwa ni viti vya enzi, au usultani, au enzi au mamlaka; vitu vyote vilivyoyumbwa kwa njia yake, na kwa ajili yake. Naye amekuwepo kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana katika yeye (Wakolosai 1:15-17)

Mwanga ni mionzi ya mfano wa Mungu katika uzuri wa uumbaji. Mungu akasema, “Iwe nuru!”¹ – na mbingu zikawa na umbo. Mahali Kristo alipozaliwa, nuru iling’aa gizani – na giza haliwezi kamwe kulishinda hili agano linalong’aa la Mungu aliye hai.²

Krismasi ni majira ya kusifu kwa nyimbo,³ ingawa hali halisi wakati huu ya uharibifu wa mazingira unaathiri sifa za Mungu katika uumbaji. Nyimbo za malaika kutoka mbinguni hazisikiki kwa ajili ya uchavuzi wa hewa na kelele za viwanda. Sauti za mawimbi baharini zinaathiriwa na mabadiliko ya hewa. Uzuri wa uhai wa viumbe umeharibiwa na vitendo vibaya vinavyotokana na ulafi. Sayari yetu inavyoteseka ndivyo wakazi wake wanavyoteseka. Tayari watu maskini na waliosahauliwa kijamii wanaona ugumu kupaza sauti zao wakiimba.

Wakati wa Maria na Yosefu, Mfalme Augusto aliamini kuwa mamlaka yote yalikuwa mikononi mwake peke yake. Alitoa amri kuwa “ulimwengu wote” ulipe kodi (neno la kibiblia la ulimwengu wote ni *oikumene*)⁴. Wakati huo jamaa ya Maria na Yosefu walifanya safari kuelekea Betlehemu. Lakini Mungu alikuwa na shabaha nyingine katika historia. Sasa tunatambua kuwa enzi, dola, watawala na mamlaka vilikuwepo na kutenda mambo ili unabii utimie. Ni Kristo na sio mfalme ambaye “amekuwako kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana naye.”⁵

Mtheologia wa biblia Barbara Rossing alisema, kuwa dola ya ki *oikoumene* ya Caesar – ikiambatana na uchumi wa kisasa, nguvu za kijeshi na ukiritimba wa kisiasa- ilitokomea. Manabii na mitume wanatuhakikishia kuwa uumbaji wa Mungu-*oikoumene* ya kweli ambayo ni makao ya Mungu utabadilika.⁶

Kwa hiyo tunaomba mabadiliko na kujitoa kuwa nyenzo za kuleta hayo mabadiliko.⁷ Tunaishi katika imani kuwa kuja kwa Kristo, kuna uumbaji mpya ambao kwa huo tumaini

¹ Mwanzo 1:3.

² Yohana 1:4-5.

³ Luka 2:14.

⁴ Luka 2:1.

⁵ Wakolosai 1:17; Zaburi 2:7-10.

⁶ Isaya 65:17; Ufunuo 21-22.

⁷ 2 Wakorintho 4:16.

lililo ndani ya nyimbo za malaika linatimilika- Mungu, binadamu na uhai wote vitapatanihwa .⁸

Rev. Dr Samuel Kobia
Katibu Mkuu
Baraza la Makanisa Duniani

This message is also available in German, French, Spanish, Korean, Arabic, Georgian, Portuguese and some other languages at the website of the World Council of Churches (<http://www.oikoumene.org/?id=7307>).

⁸ 2 Wakorintho 5:17-20.